TANGAZO LA SERIKALI Na. 360 la tarehe 19/5/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1) na (2))*

## NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KAHAMA-SHINYANGA) YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga) ya Mwaka 2023.

Kuongezwa eneo la huduma
.

2.-(1) Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga linaongezwa ili kujumuisha maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

(2) Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga Kahama Shinyanga itakuwa na jukumu la kusimamia na kuendesha miundombinu ya maji inayoimiliki na kusambaza maji kwa ujumla kwa mamlaka za maji, vyombo vya kijamii na vijiji katika eneo la huduma lililoongezwa.

*Tangazo la Serikali Na. 360 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2(1))*

| | JINA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA | ENEO LA HUDUMA LILILOONGEZWA |
|---|---|---|
| | Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga | Wilaya ya Misungwi na Wilaya ya Kwimba zilizopo Mkoa wa Mwanza; Wilaya ya Kishapu mkoa wa Shinyanga; Manisapaa ya Tabora, Wilaya ya Nzega, Wilaya ya Igunga, Wilaya ya Uyui, Wilaya ya Tabora, Wilaya ya Kaliua, Wilaya ya Urambo na Wilaya ya Sikonge katika Mkoa wa Tabora; baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Maswa Mkoa wa Simiyu; Wilaya ya Nyang'wale mkoa wa Geita; na Wilaya ya Iramba mkoa wa Singida. |

Dodoma,
5 Mei, 2023

JUMAA H. AWESO,
*Minister for Water*